BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


**MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma na utukufu kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana tena kwa lengo la kujadili masuala ya msingi yanayolihusu taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi zake anazozichukua kuwaletea wananchi maendeleo. Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri ambayo kila mtu anaiona na sisi Kamati tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya na nguvu zaidi ili aifikishe Zanzibar mbali na uchumi wetu uweze kukua zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizo za Mheshimiwa Rais, pia tunawapongeza Makamo wake wote wawili, Mheshmiwa Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa juhudi zao za kumshauri vyema Mheshimiwa Rais katika harakati zake pamoja na kujitoa kwao kuwahamasisha wananchi katika kutekeleza wajibu wao.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nichukuwe nafasi hii kwa mara nyengine tena kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi, pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipatia Kamati hii ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na shukurani hizo, Kamati pia inatoa shukurani kwa kupatiwa nafasi ya kueleza angalau kwa muhtasari, ripoti ya Kamati inayotokana na kazi zilizotekelezwa kwa takribani mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 107(1) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2020 na majukumu yake yametajwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena napenda kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha katika kipindi chote cha Kamati, ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa.

Naomba niwatambuwe Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Aza Januari Josseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Ali Abdul Gulam Hussein | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Mwanajuma Kassim | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Sada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 8. | Ndugu Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 9. | Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara pamoja na taasisi zake na baadae kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

**Mjeshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inasimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara kwa Unguja , Pemba na Dar es Salaam ikiwa na lengo la kufuatilia kwa kina utekelezaji wa miradi na shughuli za Wizara hizo ambazo hupangwa katika mfumo wa kibajeti wa Programu kama ifuatavyo:

## WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utallii katika kutekeleza majukumu yake ilifanya ukaguzi katika Programu Kuu za Wizara zifuatazo:

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo;

2. Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;

3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo;

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kusimamia matumizi sahihi ya pembejeo na utoaji wa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima, ikiwemo utoaji wa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao. Aidha, programu ina jukumu la kusimamia na kuendeleza tafiti za kilimo na maliasili pamoja na upatikanaji wa huduma za matrekta na zana za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa programu hii, kuna mafanikio kadhaa yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na kuyaendeleza baadhi ya mashamba ya viungo likiwemo shamba la viungo Kizimbani, ambapo shamba hilo limekua kwa kiasi kikubwa likiisaidia Serikali kuongeza mapato kupitia ujio wa watalii ambao huingia kwa wingi shambani na kupelekea kuongezeka kwa pato la taifa. Aidha, program pia ina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji jambo ambalo limesaidia kuwaongezea ujuzi watendaji katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kuboresha miundombinu katika baadhi ya vituo vya uzalishaji miche ya mazao na matunda kikiwemo kituo cha uzalishaji miche cha Wesha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza taasisi ya Kilimo Kizimbani kwa hatua nzuri zilizofikia katika ufanyaji wa tafiti mbalimbali zinazohusu kilimo. Taasisi imefanikiwa kupata matokeo mazuri ya utafiti wa mbegu za mpunga zinazostahamili maradhi ya manjano ***'Rice Yellow Mottle Virus'*** na ukungu ***'Rice Blast'*** kwa kutumia teknologia ya mionzi (Nuclear Radiation) na kufanikiwa kupata tuzo ya Kimataifa ya mwanasayansi bora katika uzalishaji wa mbegu za mpunga. Kamati inachukua nafsi hii kumpongeza mtaalamu wetu ndugu Salum Faki Hamad aliyetunukiwa tuzo hii kutoka Shirika la Kimataaifa la Nguvu za Atomiki ***'International Atomic EnergyAgency'*** lenye Makao yake makuu Vienna Austria mnamo mwezi Septemba mwaka 2021. Waswahili wanasema '***Mcheza kwao hutunzwa'*** Pongezi zetu pia tunazitoa kwa Wizara ya Kilimo, Umwagilaiaji, Maliasili na Mifugo kwa kupata tuzo hiyo ambayo imekua ni kielelezo tosha cha kuonesha umahiri wa wataalamu wetu ambao wamekua wakifanya kazi kubwa katika kuliendeleza taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo katika taasisi hii Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo zinakwamisha utekelezaji wa program hii. Katika ziara zake, Kamati ilisikitishwa na kiwango kidogo cha fedha za ukodishwaji wa shamba la Makuwe kisiwani Pemba, ambapo ilielkezwa kuwa kwa msimu wa karafuu uliopita shamba lilikodishwa kwa shilingi Milioni tano tu za kitanzania. Awali shamba hilo liliwahi kukodishwa kwa shilingi Milioni 300 za kitanzania.

Kamati ililiona jambo hili kuwa ni ubabaishaji uliofanywa na baadhi ya viongozi waliolenga kujipatia maslahi binafsi na kuinyima Serikali mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhika na maelezo yaliyotolewa kuhusiana na ukodishwaji huo kutokana na ukubwa wa eneo hilo lenye hekta 79.9 sawa na eka199.75 ambalo ni eneo kubwa sana na ni jambo la kushangaza kusikia shamba hilo limekodishwa kwa fedha hizo. Baada ya ziara hiyo ya Kamati Serikali ilitoa muongozo wa kusitisha ukodishwaji wa mashamba yote ya Serikali, kutokana na hasara kubwa inayopatikana katika ukodishwaji wa shamba la Makuwe, Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza sana serikali kwa hatua yake hiyo yenye lengo la kuzilinda rasilimali za taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa program hii kupitia Taasisi ya Utafiti wa kilimo, kulielezwa changamoto ya kukosekana kwa fedha za kutosha za kufanyia tafiti za kilimo. Ukosefu huo wa fedha umesababisha Taasisi hii kwa upande wa Pemba kutofanya tafiti kwa muda wa miaka mitatu sasa. Aidha ukosefu wa fedha za gawio la fedha za maendeleo kutoka Serikalini ni changamoto ambayo imekua ikisababisha kutofanywa kwa tafiti za kilimo katika kituo cha Matangatuwani Pemba. Fedha hizo zimekosekana tangu bajeti ya mwaka 2015/2016 hadi leo ambapo kituo hicho hakijapatiwa mgao wa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imesikitishwa sana na hali hiyo kutokana na ukweli kwamba tafiti zinazofanywa na wataalamu wetu ndio chimbuko la kilimo bora kwa watu wetu ambao wengi wao hali zao ni duni na hutegemea kilimo ili waweze kujikimu katika mahitaji yao ya msingi. Kamati inaishauri Serikali katika vipaumbele vyake vya mgao wa fedha, taasisi nyeti kama hizi ambazo zina majukumu makubwa kwa wananchi wetu zipewe kipaumbele kwa kupewa fedha zote zinazohitajika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa Programu ndogo ya ya kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji**,** Kamati ilifanya kikao na mabibi na mabwana shamba ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana ukizingatia na majukumu makubwa waliyonayo. Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa bibi/bwana shamba mmoja anahudumia wakulima hadi 2000 wakati anatakiwa kuhudumia wakulima 300 hadi 350. Hali hii inawapelekea watendaji hao kutofanya kazi kwa ufanisi na hatima yake ni kilimo kisichokuwa na tija kwa wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kisiwa cha Pemba, kwa sasa kuna mabibi / mabwana shamba 21 tu wakati wanaohitajika ni 129, takwimu hii ya kisiwa cha

Pemba ni kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa katika ziara ya Kamati iliyofanyika katika bonde la umwagiliaji la Saninga tarehe (8/11/2021). Kupitia ripoti hii, tunaiomba Serikali iliangalie tena suala hili kwa kuhakikisha kuwa itakaporuhusu ajira basi na suala la mabibi na mabwana shamba lizingatiwe.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu na ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao, kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali misitu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa programu hii, Kamati ilifurahishwa na mafanikio yaliyopatikana ambapo Idara ya Misitu imeweza kuweka uhusiano mzuri na wana vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi ya msitu wa Jozani kwa kugawanya asilimia kadhaa ya mapato kwa wanavijiji hao kupitia Kamati zao walizoziunda wenyewe ambazo zimekua mstari wa mbele katika kuhamasisha uhifadhi wa maeneo yote ya msitu. Idara kwa kushirikiana na Kamati za wana vijiji zinafanya juhudi kubwa ya kubuni vivutio vipya ndani ya misitu ambavyo vitasaidia kuongezeka kwa mapato na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea misitu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kufanya uchunguzi mdogo imegundua kuwa mafanikio yaliyopatikana ya kugawana asilimia kadhaa ya mapato imeingia dosari baada ya mapato hayo kwa sasa kukatwa kwa 25%. Kamati imebaini kuwa awali fedha hizo zilikuwa zikikusanywa na kufanywa mgao sehemu mbili ambao ni baina ya Idara ya Misitu na wanakijiji wanaozunguka maeneo yam situ. Kamati imeelezwa kuwa fedha hizo zimeanza kukatwa kuanzia mwezi July-Desemba, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua nafasi hii kushauri fedha hizo zisikatwe na badala yake urudishwe utaratibu ule ule uliokua ukifanyika kipindi cha nyuma. Kamati inayasema haya kutokana na wingi wa shughuli za maendeleo

walizojipangia wananchi hao na fedha hizo kutokidhi mahitaji yote. Tunaamini Serikali itakisikia kilio hiki cha wananchi na kuzirudisha fedha hizo ili tuwape moyo wananchi wanaojitolea kulinda rasilmali za msitu wetu.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO**

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Katika utekelezaji wake programu imefanikiwa kuanzisha kituo cha kuhifadhia gesi ambacho pia kinahifadhi mbegu za ng'ombe wa sindano kilichopo Maruhubi Unguja. Kituo hiki kwa kiasi kikubwa kimekua ni tegemeo kwa wafugaji wetu katika shughuli zao za ufugaji. Aidha, kwa sasa kituo kina mtambo wa kuzalisha gesi za upandishiaji wa ng'ombe wa sindano jambo ambalo limefurahiwa sana na wafugaji wetu ambao wamekua wakitegemea huduma za kituo katika uzalishaji wao.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kubwa katika utekelezaji wa programu hii ni uchakavu wa mtambo wa kuzalishia gesi ambao ni wa muda mrefu hali inayopelekea kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa gesi jambo linalopelekea kushuka kwa uzalishaji wa ng'ombe wapya.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo Kamati inaishauri Serikali kununua mtambo mwengine mpya wa kuhifadhia gesi na kuachana na kuufanyia matengenezo mtambo uliopo sasa hasa ikizingatiwa kuwa mtambo huo ni wa muda mrefu na vifaa vyake vimeshachakaa. Kuendelea kuufanyia matengenezo mtambo huo ni kujitia hasara. Hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Idara ya Maendeleo ya Mifugo kufanya haraka kuandika waraka Serikalini na kuelezea mahitaji ya kununua mtambo mpya kwani waswahili wanasema '***kata pua uunge wajihi***'. Kamati inaishauri Serikali ijipange kwa hali yoyote ile kwa lengo la kutafuta fedha na kununua mtambo mpya ili kuepuka hasara inayoendelea kupatikana siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipofanya ziara kisiwani Pemba katika kikundi cha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kilijionea mafanikio ya wafugaji hao ilielezwa kuwa idadi ya lita za maziwa kutoka lita 20 hadi lita 70 kwa siku ndizi zinazozalishwa kutokana na elimu nzuri ya kitaalamu waliyoipata kutoka katika Idara ya Mifugo. Ilielezwa kuwa wafugaji hao wamefanikiwa kuwaelemisha wafugaji wenzao wa maeneo ya karibu jambo lililopelekea ushirikiano wa hali ya juu hasa katika suala zima la ulinzi wa mifugo. Baada ya kusikia changamoto

ya soko la maziwa ya wagugaji wetu, Kamati inaishauri Serikali kufanya juhudi za haraka na za makusudi kutafuta soko la uhakika la kuuzia maziwa yanayozalishwa na wafugaji wetu kwa kutafuta wafadhili wa kununua maziwa hayo wakiwemo wawekezaji wazawa waliopo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea maeneo kadhaa ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuona juhudi zao kubwa wanazozichukua katika uzalishaji wa maziwa lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hadi wakati huu, maziwa yanayozalishwa na wafugaji hao yamekua yakiuzwa kwa bei ya chini jambo ambalo linawaumiza wafugaji wetu na kuwakatisha tamaa. kwa mfano, wagujaji wa kikundi cha Piki/Tundwa ambako Kamati ilipata nafasi ya kuwatembelea wafugaji wale ilielezwa kuwa takribani lita 70 za maziwa huzalishwa kila siku wakati huo huo kuna changamoto nyengine ya kukosekana kwa mafriza ya uhakika na majenereta ambayo yangeweza kutumika katika uhifadhi wa maziwa pindi inapohitajika kufanya hivyo. Ilielezwa kuwa kwa sasa kuna tatizo kubwa la upungufu wa mafriza ya kuhifadhia maziwa ambapo mafriza yaliyopo hivi sasa hayakidhi mahitaji.

**PROGRAMU NDOGO YA KUENDELEZA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI**

**Mheshimiwa Spika,** programu hii ililenga kujenga misingi mikubwa na midogo ya kumwagilia maji katika mabonde ya Kinyasini, Kibokwa na Chaani pamoja na kufanya majaribio ya utokaji wa maji katika mabonde ya Cheju na Kiliombero. Katika utekelezaji wa program hii, Kamati ilijionea mafanikio makubwa yaliyopatikana katika miradi ya umwagiliaji katika bonde la Cheju na Kilombero.

**Mheshimiwa Spika,** miradi hiyo ilikua imekamilika kwa aslimia 80% kipindi ambacho Kamati iliitembelea. Kutokana na juhudi kubwa za Serikali yetu, Kamati ya Kilimo, Biashar ana Utalii inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali na Wizara kwa ujumla kwa juhudi zake za kuisimamia vyema miradi hiyo na kuhakikisha fedha iliyopangwa inatumika ipasavyo.

**Mheshimiw Spika,** pamoja na mafanikio hayo kulikuwa na changamoto kadhaa zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi hiyo ambapo iliibainika changamoto ya uharibifu wa baadhi ya miundombinu ya umwagiliaji inayofanywa na baadhi ya wananchi wasioitakia mema nchi yetu Kamati ilisikitishwa sana na kuona uharibifu wa miundombinu hiyo ambayo mengine tayari imeshakamilika na imegharimu fedha nyingi. Ilielezwa kuwa baadhi ya wananchi kuchimba mchanga, kufunga wanyama ndani ya maeneo ya mradi na baadhi yao kuzitumia njia zilizojengwa kwa lengo la kusafirishia mazao kwa

shughuli zao binafsi ikiwemo kupitisha magari ya mchanga wa wizi jambo ambalo linaharibu miundombinu hiyo iliyojengwa kwa gaharama kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kujione uharibifu huo, ilichukua hatua ya kukutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kaskazini 'B' na kujadiliana suala hilo ambapo majadiliano ya kikao hicho yalifikia muwafaka wa kuitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kushirikiana kikamilifu na Kamati zote za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mkoa kwa maeneo yote yenye miradi kwa lengo la kuongeza ulinzi wa maeneo hayo na kuokoa fedha za Serikali zinazotumika katika miradi hizo. Kupitia taarifa hii, Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii inapenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Ulinzi na Uslama ya Wilaya ya Kaskazini 'B' kwa kuitikia wito wa Kamati na kuahidi kuchukua hatua za haraka za kulinda miradi ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazidi kusisitiza na kuiagiza Wizara ya Kilimo kutoa taarifa zote za mradi kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama na kuwshirkisha katika mambo yote yanayohusiana na mradi. Aidha, Kamati inaendelea kutoa ushauri kwa Serikali na Wizara kwa ujumla kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kujipatia maendeleo enelevu kwa maslahi ya taifa letu. Ikukmbukwe kwamba wataalamu waliwahi kutwambia '***Hawawi sawa wale waliosoma na wale wasiosoma***', hivyo ni vyema Wizara ikaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuilindwa miradi hiyo na hatimae kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa na Serikali.

## WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utallii katika mkutekeleza majukumu yake ilifanya ukaguzi katika Programu Kuu za Wizara zifuatazo:

i. Programu kuu ya ukuzaji na uendelezaji wa biashara
ii. Programu Kuu ya Uendelezaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Mendeleo ya Viwanda

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa programu hii mafanikio kadhaa yalibainika na Kamati ambapo kupitia Tume ya Ushindani Halali wa Biashara imefanya ukaguzi katika maduka mbali mbali hapa nchini na kufanikiwa kukamata bidhaa zilizoisha muda wake. Miongoni mwa bidhaa hizo ni pamoja na vyakula vya makopo, kemikali na bidhaa za matumizi ya nyumbani ambazo muda wa matumizi yake umeshapita.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika ziara zake pamoja na mafanikio hayo yaliyopatinaka katika utekelezaji wa program hii kupitia Tume ya Ushindani Halali wa Biashara, Kamati ilifanya ziara ilielezwa kuwa Tume inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi wa kutosha hasa kisiwani Pemba ambapo Tume ina wafanyakazi watano tu. Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali itakapotoa ruhusa ya ajira Tume nayo iruhusiwe kuajiri kwa lengo la kuondoa changamoto hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ilielezwa kwa sasa majengo ya Tumne yanayotumika kwa shughuli za kiofisi ni ya kukodi, hivyo Kamati inaishauri Serikali iendelee na juhudi inazozichukua za kujenga majengo mapya na ya kisasa kwa matumizi ya ofisi. Tume ya Ushindani Halali wa Biashara ni miongoni mwa Taasisi nyeti zilizopo hapa nchini, hivyo inastahili kupatiwa eneo zuri lenye mazingira tulivu ya kufanyia kazi.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogovidogo, vidogo na vya kati (SMIDA), ikiwa na lengo la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera ya maendeleo ya viwanda nchini, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa programu na mikakati

ya maendeleo ya viwanda na kufuatilia ukuaji wa sekta ya viwanda na utendaji wake kwa kubaini vikwazo vinavyoikabili sekta hiyo na kuchukuwa hatua za kuziondoa.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa programu hii, kuna mafanikio yaliyopatikana yakiwemo ya kufuatilia ukuaji wa sekta ya viwanda na utendaji wake kwa kubaini vikwazo vinavyoikabili sekta hiyo na kuchukuwa hatua za kuviondoa. Kutokana na juhudi hizo zilizochukuliwa na Idara ya Maendeleo ya Vianda, kasi ya uwekezaji nchini imeongezeka na kwa msasa kisiwani Pemba Serikali kwa makusudi imetenga eneo maalum la uwekezaji katika eneo la Chamanangwe. Hatua hii inalenga kutanua wigo katika sekta ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** juhudi za Idara hii zimeweza kuleta matunda mazuri ambapo kwa sasa kisiwani Pemba katika eneo la Chamanangwe kuna muwekezaji mzalendo amejitokeza na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha maji kiitwacho **AMOS INDUSTRIAL LTD** ambacho kwa sasa kipo hatua ya mwisho ya maandalizi ya uzalishaji. Kamati inaamini kuwa uwepo wa kiwanda hicho, utasaidia kupunguza makali ya ajira kwa vijana wetu wengi ambao malalmiko yao makubwa ni ukosefu wa ajira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali pamoja na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa juhudi ilizozichukuwa kulifanikisha suala hilo, Kamati inaamini kuwa endapo Idara itaendelea na juhudi zake hizo, eneo la uwekezaji Chamanangwe litaibua fursa kwa wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza hapa nchini na litakua ni eneo la mfano kwa hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo makubwa yaliyopatikana bado kuna changamoto katika sekta hiyo ambapo Kamati ilibaini changamoto ya kuwepo kwa baadhi ya wananchi wanaokataa fedha za malipo ya fidia zilizokadiriwa na Serikali kwa madai kuwa fedha hizo ni kidogo na hazilingani na thamani ya maeneo waliyoyatoa. Kamati baada ya kupata maelezo ya kina kuhusiana na suala hilo inaishauri Wizara kufanya juhudi maalum za kuhakikisha kuwa inaweka kumbukumbu zote vizuri zinazohusiana na eneo hilo kwa lengo la kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza hapo baadae kutokana na baadhi ya wananchi hao hao wanaokataa fidia zao, baadhi yao kujitokeza kwenda kuchukua fidia hizo kinyemela pasi na kuwajuulisha wenzao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inayasema haya kutokana uzowefu unaoonesha kuwa baadhi ya wananchi huitumia nafasi kama hii kwa kufanya udanganyifu

na hatimae kuweza kupatiwa fidia mara mbili au zaidi, hivyo tunapaswa kuuzingatia msemo wa Kiswahili usemao '***Mali bila ya daftari hupotea bila ya habari'.***

**SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika Shirika la Biashara la Taifa kwa Unguja, Pemba na Dar es Salaam na kujiona maendeleo ya Shirika hilo pamoja na kukagua baadhi ya maghala ya kuhifadhia karafuu kwa Unguja, mashine za shirika katika kiwanda cha Makonyo Pemba, kukagua baadhi ya majengo ya shirika ambayo kwa sasa yanatumika kama kitega uchumi cha Shirika Unguja na Dar es salaam, pamoja na nyumba ya Shirika iliyopo Sinza.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika liliieleza Kamati kuwa katika kipindi cha miaka kumi ya mageuzi (**2011/2012 – 2020/2021)** limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuchangia katika uchumi wa Taifa kutokana na ongezeko la 58.5% ya mauzo ya karafuu ambapo Shirika limeweza kupata faida ya shilingi Bilioni 512 wakati huko nyuma Shirika lilikuwa likipata shilingi milioni 68 tu. Aidha, katika kipindi cha miezi sita Shirika limefanikiwa kupeleka Serikalini shilingi Bilioni 120 kwa lengo la kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa Shirika kama hili na sisi Kamati tunalipongeza sana Shirika hili na tunatoa wito kwa Serikali na wadao wote kwa ujumla, ni vyema Shirika hili likajiendesha kitaalamu ili liweze kupiga hatua mbele zaidi ya hapo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inatoa pongezi hizo kwa dhati kabisa kwa kuzingatia na hasara kubwa inayobebwa na Shirika hili kutokana na mzigo mkubwa inaoubeba kutokana na kuchangia kuongeza bei ya karafuu pamoja na kuchangia katika mfuko wa maendeleo ya karafuu ambapo kuna wadau kadhaa waliotajwa katika Sheria lakini wadau hao hawatoi kitu na mzigo wote unabebwa na Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mzigo unaobebwa na Shirika la Biashara ambao ulisababisha deni kubwa kwa Shirika hili ambapo tarehe **06/04/2021** Kamati ilifanya ziara kwa mara ya kwanza katika Shirika hili na kuelezwa kuwa Shirika linakabiliwa na madeni makubwa ambayo yamekua ni mzigo mzito sana kutokana na mambo mengi yanayohitajika kutekelezwa. Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya taasisi za Serikali na binafsi zinalidai Shirika hilo. ikiwemo ZSSF wanaodai shilingi bilioni 5, PBZ shilingi bilioni 8, wateja wa karafuu shilingi bilioni 6.7, ZECO shilingi milioni 708 na Selem Construction shilingi milioni

1.1. Wizara ya Vijana shilingi milioni 377, 000, 000,00, madeni ya kiinua mgongo kwa wafanyakazi waliostaafu shilingi Milioni 225.

**Mheshimiwa Spika,** madeni yote haya yaliathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa baadhi ya miradi ukiwemo ujenzi uliokuwa ukifanywa na kampuni ya Selem Construction kisiwani Pemba ambao mradi huo ulisita katika hatua ya msingi kutokana na ukosefu wa fedha na deni lililopo.

**Mheshimiwa Spika,** kikao cha tarehe **13/02/2022** baina ya Kamati na Shirika kilieleza kua baadhi ya madeni hayo yameshalipwa yote na kwa sasa Shirika linadaiwa na taasisi mbili tu ambazo ni ZSSF wanaolidai shilingi shilingi bilioni 5 na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) wanaodai shilingi bilioni 8. Kupitia taarifa hii tunalipongeza sana Shirika letu la biashara kwa juhudi kubwa walizozichukua na tunayao,mba mashirika mengine ya Serikali yaige mfano wa Shirika hili kwa kwenda kuchota mbinu wanazozitumia katika kupamba na matatizo yao pamoja na kuongeza mapato wanayoyakusanya.

**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utallii katika kutekeleza majukumu yake ilifanya ukaguzi katika Programu Kuu za Wizara hii zifuatazo:-

1. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya kale na uhifadhi wa Mji Mkongwe;
2. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii;
3. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE**

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajumuisha program ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Programu ndogo ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo na maeneo ya kihistoria kwa lengo la kuona maendeleo yake pamoja na tija inayopatikana kupitia maeneo hayo. Kamati ilipata nafasi ya kukagua jengo la Baitul Ajaib liliopo Forodhan na kujionea hali halisi ya maendeleo ya ukarabati wa ujenzi uliotokana na kuporomoka kwa jengo hilo. Kamati imeridhika na hatua ya kwanza ya maendeleo ya ukarabati huo na inachukuwa nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa juhudi kubwa ilizozichukuwa za kulinusurru jengo hilo lisije kumalizika na kupoteza muonekano wake wa awali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ziara hiyo, Kamati pia ilipata nafasi ya kuyatembelea maeneo mengi ya kihistoria Unguja na Pemba, ambayo maelezo yake ya kina yapo katika ripoti kuu na hapa tutaeleza kwa uchache tu kuhusiana na maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** katika maeneo mengi ya kihistoria ambayo Kamati iliyatembelea ilibaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya kukosekana kwa hati miliki ya maeneo hayo pamoja na uvamizi mkubwa unaofanywa na baadhi ya wananchi kwa shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kilimo na makaazi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa sana Kamati inaeleza changamoto hii ambapo ilielezwa kuwa suala la upatikanaji wa hati miliki limekuwa na changamoto kubwa kwa maeneo mengi ya kihistoria kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Ardhi imekuwa ni kikwazo kikubwa sana katika upatikanaji wa hati miliki hizo kwa maeneo mengi ya kihistoria. Ilielezwa kuwa tokea mwaka **2006** hadi **2007** ni maeneo **14** tu yaliyopatiwa hati miliki kati ya maeneo **86**. Maeneo hayo yote yapo Unguja na kwa upande wa Pemba hakuna eneo hata moja lililopatiwa hati miliki. Kamati ilisikitishwa sana na taarifa ya kuwa kuna baadhi ya maeneo yalitolewa fedha na wafadhili kwa lengo la kupimwa na kupatiwa hati miliki lakini kutokana na kucheleweshwa na kuzungushwa kwa kufanywa vipimo hivyo na Wizara ya Ardhi, baadhi ya wafadhili hao wamechukua fedha zao.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hili halivumiliki na halikubali hasa tukizingatia kuwa taasisi zote hizi ni za Serikali. Hivyo, Kamati inachukua nafasi hii kuishauri Serikali kutoa agizo kwa Wizara ya ardhi kuwachukulia hatua wale wote waliohusika na ucheleweshwaji huo pamoja na kuwahimiza kutoa hati miliki kwa maeneo yote muhimu ya Serikali ili kuepusha uvamizi unaoendelea kufanywa na baadhi ya wananchi katika maeneo mengi ya kihistoria. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufuatilia mara kwa mara suala hili hasa katika maeneo ambayo tayari wamekwisha yaombea hati miliki.

## PROGRAMU KUU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII

**Mheshimiwa Spika,** programu hii imelenga kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusiana na bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Aidha, progamu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeundwa kwa Sheria namba 9 ya mwaka 1996 ambayo ilifutwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2009. Kwa sasa Kamisheni ya Utalii inaendeshwa kwa kufuata Sheria No.6 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na.7 ya mwaka 2012.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kuandaa na kushiriki maonesho, mikutano na makongamano ya Utalii ya kitaifa na kimataifa ili kuvutia wageni waweza kuvitembelea vivutio vya Utalii vya Zanzibar. Programu hii kupitia Kamisheni ya Utalii, imefanikiwa kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri kwa lengo la kuipatia Zanzibar fursa ya kutangazwa kupitia watu hao kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamisheni pia imefanikiwa kuandaa na kutoa matangazo ya utalii katika majarida, televisheni za kitaifa na kimataifa na mabango ya kielektroniki ili kuwavutia watalii wengi zaidi kutoka katika masoko ya asili na mapya.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, Kamisheni inakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa maeneo ya kihistoria hali inayopelekea kuharibu uasili wa maeneo hayo pamoja na changamoto ya ya uhaba wa fedha wa

kuendeshea shughuli za Kamisheni jambo ambalo linaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa mipango inayopangwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipatiwa taarifa ya kwamba fedha zote zinazokusanywa na Kamisheni ya Utalii zinapelekwa hazina jambo ambalo sio baya kama taratibu zinavyoelekeza. Hata hivyo, Kamati kupitia taarifa hii inaiomba Serikali kulifikira suala la kubakisha japo asilimia ndogo ya makusanyo hayo, ambapo Kamati minapendekeza isipungue 25% ya mapato kwa Kamisheni ya Utalii ili baadhi ya changamoto ziweze kutatuliwa kwa wakati hasa tukizingatia jukumu zito la Kamisheni katika sekta ya Utalii. Kamati inaamini kuwa, kubakishwa kwa fedha hizo kutaifikisha Zanzibar sehemu nyengine ya mbali zaidi katika Utalii ambao ni miongoni mwa vianzio vikuu vya uchumi wa Zanzibar.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii imejikita zaidi katika kukagua miradi ya maendeleo ambayo bajeti yake tuliipitisha katika Baraza hili na sisi kama Kamati, tulizifanyia kazi program zote ambazo zina miradi ya maendeleo. Kamati imetoa mapendekezo na maagizo mbali mbali ambayo ni matumaini yetu kuwa yatafanyiwa kazi na mwezi Septemba mwaka huu Wizara zote zitakuja na maelezo ya kutujibu kuhusiana na utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, naomba nikushukuru na niwashukuru tena Wajumbe wako kwa utulivu wao wa kuniskiliza wakati wa kuwasilisha muhtasari huu wa ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii.

**Mheshimiwa Spika**, ahsante na naomba kutoa hoja.

**Ahsante,**

**Yussuf Hassan Iddi,**

**……………………………..**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar.</u>**